# KENYA NATIONAL EXAMINATION COUNCIL
# REVISION MOCK EXAMS 2016
## TOP NATIONAL SCHOOLS

**BAHATI GIRLS HIGH SCHOOL**
**KISWAHILI**
**KARATASI YA 3**
**MWONGOZO WA KUSAHIHISHA**

**SCHOOLS NET KENYA**
Osiligi House, Opposite KCB, Ground Floor
Off Magadi Road, Ongata Rongai | Tel: 0711 88 22 27
E-mail:infosnkenya@gmail.com | Website: www.schoolsnetkenya.com

# BAHATI GIRLS HIGH SCHOOL KCSE TRIAL AND PRACTICE EXAM 2016

**102/3**

**Karatasi ya 3**

**MWONGOZO WA KUSAHIHISHA**

1. **SEHEMU YA A – USHAIRI**

(a)

- Anahimiza matumizi bora ya Kiswahili miongoni mwa vijana na mabenati.
- Kuonyesha jinsi vijana wa Nairobi / Jijini hutumia Kiswahili kwa njia isiyofaa / isiyoeleweka na wazee / wengi.
- Kuonyesha jinsi vijana wa mjini walivyopotoka kimaadili. (1x2= alama 2)

(b)

(i) Vina – Ukara
Vina vya ukwapi vinabadilika ilhali vya utao vinatiririka ubeti hadi mwingine.

(ii) Vipande – Mathnawi

- Kila mshororo umegawika katika vipande viwili: ukwapi na utao. (2x2= alama 4)

(c)

- Matumizi ya sheng' lugha ya mtaani k.m. ushago, madhee, fadhee, doo.
- Utohozi – deti, taimu, fudi, sigareti n.k.
- Kuboronga sarufi / sintaksia ngeni.
- La kusema silipati – silipati la kusema.
- Kipi Kiswahili hiki – Kiswahili hiki ni kipi
- Ni huu ndio wakati – wakati ndio huu.

- Inkisari – wenda – unaenda. yu – yuko. Idhini na mfano. (2x2= alama 4)

(d) Tashbiha / Tashbihi

- Mkali kama ghosti.

- Maswali balagha

- Kibwagizo …kipi Kiswahili hiki. (2x2= alama 4)

(e) Mshairi anasema kuwa alibaki

(i) kudangana / kutafuta na hakupata la kusema. Anaendelea kusema kuwa lugha zao hazikulingana /kufanana hata kidogo.

(ii) Anaongeza kuwa hali hii iliwafanya wasielewane.

(iii) Hadi benati alipoondoka. Anasisitiza kwa kuwauliza vijana na mabenati aina ya Kiswahili

(iv) Wanachokitumia. (4 x 1 = alama 4)

(f) (i) Shababi – kijana.
(ii) Mikogo – maringo / majitwezo / mashobo / majitapo / majishawo. (1 x 2 = alama 2)

2. **RIWAYA**

(a) Msemaji – Mtemi Nasaba Bora.
Msemewa – Amani
Mahali – Sebuleni katika kasri la mtemi / nyumbani mwa mtemi.
Kisa – Baada ya Amani kumwokoa. Mtemi Nasaba Bora asilipuliwe na Gaddafi na kumfanya aungame maovu yake. (4x1 = alama 4)

(b) Tashihisi / uhuishaji – wema wako umeniua.
Jazanda – moyo kuwa mahakama. Kutaja 1, mfano 1 (2 x 2 = 4) za kwanza mbili

(c)

- Wizi wa mashamba ya wanyonge – Chichiri Hamadi, mamake Imani.

- Uzinifu / uasherati – Lowela / Kushiriki mapenzi na msichana mchanga.
- Kusingizia watu makosa / kutoa hongo – Yusuf Hamadi.
- Mapigo – Amani / Kumpiga Amani kikatili.
- Kumpagaza Amani mzigo – mtoto Uhuru.
- Anawafungia Amani na Imani korokoroni bila makosa.
- Amtaliki mkewe kwa shutuma tu – mke amekuwa mwaminifu.
- Anawafuta wafanyakazi wake kiholela.
- Kuficha faili katika wizara ya ardhi.
- Kumficha Lowela ilhali wazaziwe wanamtafuta.
- Hakuchanja mbwa wake – hakujali Dj alipoumwa na Jimmy.
- Alifuja pesa za kujengea hospitali – akajenga zahanati.
- Hakumjali mama anayejifungua kando ya barabara. (kutaja-1, kueleza1) (6x2 = alama 12)

3. **RIWAYA**

(i) <u>Mwenye utu</u>

- Anampa Dj SHATI.
- Alikubali kuandamana na Imani hadi Sokomoko.
- Aliokoa maisha ya Mtemi – kulipuliwa na Gaddaffi.
- Aligawia maskini shamba – k.m. Dj.
- Alikubali kukilea kitoto alichokiokota.

(ii) Mzalendo Halisi

- Alihudhuria sherehe ya siku ya wazalendo.
- Alishrikiana na Madhubuti kukomboa Tomoko.
- Alimkabili Mtemi na kumkosoa dhidi ya udhalimu.
- Anahimiza watu kutokubali dhuluma.

(iii) Msiri

- Hakumwambia Imani sababu ya kutafuta ajira Sokomoko.
- Hakumwambia yeyote kuwa aliwahi kusoma hadi chuo kikuu ila Madhubuti alipogundua ujuzi wake.
- Alijua kuwa Mtemi ndiye aliyemuua babuye na kumfungisha Yusuf – hakamwambia yeyote.
- Alijua kuwa mwalimu Majisifu ndiye aliyeiba mswada wake na kuchapisha; aliiweka siri.
- Alimficha Imani asili yake.

(iv) Ni msamehevu.

- Alimsamehe Mwalimu Majisifu kwa kumwibia mswada.
- Alimsamehe Mtemi – baada ya kumpiga na kuiba shamba.

(v) Ni mtetezi wa haki / mkombozi

- Anapinga dhuluma zilizofanyiwa wanyonge.
- Aliwarudishia walionyang'anywa mashamba yao.
- Aliwahimiza watu kutokubali dhuluma – hotuba yake.

(vi) Ni jasiri

- Alimwokoa Mtemi asilipuliwe na Gaddafi.
- Alimwambia Gaddafi ampige risasi.
- Alimkabili Mtemi kwa maswali mazito.
- Kuvunja mwiko na kunywa maji ya mto Kiberenge pamoja na Imani.

(vii) Ni kijana mpole

- Hakujibizana na askari alipokuwa seli.
- Alifanya kazi kwa Mtemi kwa unyenyekevu.
- Alikaa kwa upole kwa mwalimu Majisifu na kusoma vitabu.
- Aliwasihi wauguzi katika hospitali ya Nasaba Bora wamtibu mtoto Uhuru.

(viii) Mwenye bidii

- Alisoma na kupita mitihani – akaenda chuo kikuu.
- Alifanya kazi kwa bidii kwa Mtemi – akapendwa na Zuhura na wafanyakazi wengine.

(ix) Mchunguzi / jasusi hodari

- Alifanya ujasusi wa kina na kulikomboa shamba la babuye.
- Alichunguza na kuthibitisha kuwa Mtemi ndiye aliyemfunga Yusufu.

(x) Mvumilivu

- Alichukua miaka mingi kufanya uchunguzi kuhusu wizi wa shamba la babuye, kufungwa kwa amu yake, na mswada wake.

(xi) Ni msomi

- Alielewa maana na lengo la elimu.

- Alipita mtihani.

- Alifika chuo kikuu.

- Alivichambua vitabu vya fasihi – alilinganisha na maisha halisi ya jamii.(zozote 10x2 = 20)

TANBIHI: Mtahiniwa atoe sifa na mfano wake.

4. **MSTAHIKI MEYA**

(a) Msemaji – Diwani wa I
Msemewa – Meya, Diwani II
Mahali – ofisini mwa meya.
Sababu / kisa – Baada ya wafanyakazi wote wa baraza kugoma walipokuwa wanawatarajia wageni.
(alama 4x1 = alama 4)

(b)

- Ni kibaraka / kikaragosi – anakubaliana na mikakati yote ya Meya pasi kuuliza swali.

- Msaliti – kutoa ushauri mbaya bila kujali raia.

- Fisadi – kushiriki katika kuidhinisha malipo ya ‘overtime’, hataki kulipa kodi.

- Mwenye mtazamo finyu / asiyeona mbele – Haoni mantiki katika maelezo ya Diwani wa III kuwaza kuhusu vitu vidogo – mavazi. (za kwanza mbili) (1 x 2 = alama 2)

(c)

- Kupuuzwa kwa wafanyakazi / Meya hataki kufanya mazungumzo – ‘diary’ ya Meya imejaa. Meya hataki mazungumzo / Hayuko tayari kuzungumza na wawakilishi wa wafanyakazi.

- Diwani wa I na II wanashindwa kuwajibika kama washauri wa Meya. Wanashiriki katika njama za kulifilisi baraza.

- Uundaji wa kamati nyingi – unachangia gharama zaidi kwa baraza la mji.

- Meya anafanya maamuzi mabaya ya kifedha.

- Meya anaidhinisha malipo kwa watu wasio wafanyakazi wa baraza. Bili, mhubiri.

- Meya anadunisha huduma zilizopo – elimu / matibabu – anawasomeshea wanawe ng'ambo, mkewe kujifungulia ng'ambo.

- Meya anapuuza ushauri wa Diwani wa III kuhusu maswala ya fedha – kodi, nyongeza.

- Wanataaluma kama Siki kutoshiriki katika maswala ya siasa. Wasio na elimu / ujuzi ndio hutawala – Meya.

- Meya kumshauri mwanakandarasi wa awali kulishtaki baraza la mji – analimbikizia baraza deni.

- Usimamizi wa baraza umeshindwa kuwahalikishia wafanyakazi mazingira bora ya kufanyia kazi. Waosha vyoo hawana glavu.

- Viongozi kutowaongezea wafanyakazi mshahara licha ya kupanda kwa gharama ya maisha.

- Meya anacheka na kufurahi wakati askari wanawapiga waandamaji risasi na kuwatawanya – matumizi mabaya ya vyombo vya dola / ukosefu wa usalama.

- Wanaoandamana (kwa utulivu) wanaitiwa askari badala ya kushughulikiwa / kunyima wafanyakazi haki ya kugoma.

- Viongozi wanaendeleza wizi wa mali ya umma badala ya kupinga – kuiba ardhi, kuuza fimbo.

- Viongozi wanakosa kutekeleza ahadi walizowatolea raia waliowachagua.

- Viongozi wanafisidi nchi kwa kutengeneza mipango ya kimilenia ambayo hawazingatii / viongozi kutozingatia mipango ya maendeleo,

- Meya anawafanya wanacheneo kuwa wategemezi wa misaada.

- Viongozi wanasababisha kuzorota kwa hali ya usafi Cheneo kwa kutoshughulikia maslahi ya wafanyakazi. (zozote x2 = alama 14)

5. **<u>MSTAHIKI MEYA</u>**
   Sababu za kuonyesha kuwa hakustahiki / hakufaa.

- Ubinafsi / tamaa – kuchukua vipande vya ardhi na kuwagawia rafikize / madiwani kutolipa kodi.

- Vitisho kwa wafanyakazi badala ya kuwasiliana nao vizuri. Kufuta kazi / kushinikiza raia wamuunge mkono.

- Kuajiri kwa mapendeleo / ubaguzi – mhazili wake – ufisadi.

- Baraza kukosa mahitaji muhimu – dawa, maji safi, chakula.

- Matumizi mabaya ya mamlaka / cheo – kulipa Bili, mhubiri.

- Kushiriki wizi wa mali ya umma – ardhi, fimbo.

- Kuhusisha marafiki katika uongozi wa baraza – Bili.

- Kukubali nyongeza ya mishahara ya madiwani / hakujali wafanyakazi.

- Ubadhirifu / ufujaji wa mali – divai, mvinyo. Kupeleka watoto ng'ambo.

- Kubagua / kupendelea / kutenga viongozi – Diwani III.

- Hakuviinua viwango vya elimu na matibabu Cheneo – anapendelea ng'ambo.

- Meya anapuuza ushauri wa wataalamu wa maswali mbalimbali / kuwatenga washauri bora.

- Wafanyakazi hawathaminiwi – mishahara duni, kuchelewa.

- Ametelekeza raia / hajali maisha / hali za wanyonge – mama Dadavuo.

- Mkosa utu / huruma – hajali vifo vya raia – 'mmoja tu.'

- Wananchi wanyonge wanalazimishwa kutoa kodi – madiwani wanatengwa.

- Meya ameshindwa kuwapa ajira raia wake – vijana wengi wamefuzu lakini hawana ajira.

- Kutotimiza ahadi / udanganyifu / propaganda.

- Matumizi mabaya ya vyombo vya dola – askari na vyombo vya habari.

6. **<u>SEHEMU YA D</u>**

- Kubaguliwa na wazungu – basi linampita
- Wahadhiri wanawanyima alama.
- Jaji anamtoza faini ya juu kuliko kawaida.
- Kutozwa faini wanapofanya makosa madogo k.m. kutofunga zipu.
- Kushtakiwa na kufungwa gerezani.
- Kuhadaiwa na kuporwa mali – alivyofanyiwa na Fiona / Bob.
- Baridi kali – hawakuzoea.
- Kushukiwa kuwa wezi – akiwa duka la jumla.
- Kuonewa k.m. kupewa alama chache katika mitihani vyuoni.
- Kutazamwa kwa dharau – mikahawani (aliposahau kufunga zipu).
- Kuulizwa maswali ya kukera / kuchosha kuhusu waafrika wenzao – mwaishi mitini kama tumbili.
- wasichana wenu wanakeketwa.
- Kulazimishwa washiriki ngono k.m. alivyofanyiwa na Fiona. (zozote 10x2 = 20)

7. (a) Msemaji – Bwana mmoja.
Msemewa – Msimulizi / Abu
Mahali – Mlangoni / kwa akina Amali.
Sababu / kisa – Hakutaka 'dadake' atoke kwao bila yeye kupewa kitu. (4 x 1 = alama 4)

(b)

- Mwenye tamaa ya mali – anaomba pesa msimulizi.
- Mbinafsi – angetaka afaidike binafsi.
- Mwongo / laghai – si kakake halisi wa Amani. (1 x 2 = alama 2) (za kwanza mbili)

(c) (i) <u>Umaskini</u>

- Kijijini mwa msimulizi kila mtu alikuwa maskini. Hakuna aliyeweza kumsaidia mwingine.
- Awali (miaka saba) msimulizi alikuwa fukara.
- Pesa ya msimulizi ilikataliwa mwanzoni – hangeweza kulipia mahari, kumlisha mke.

(ii) Tamaa ya mali

- Bwana aliyemzuia msimulizi mlangoni.
- Msimulizi alipewa orodha ndefu ya vitu vya thamani alivyohitajika kununua ili amwoe Amali.
- Msimulizi anakubaliwa kumwoa Amali – sasa ana mali.

(iii) Utabaka

- Maskini hana ruhusa ya kuoa kutoka tabaka la juu / kati.
- Msimulizi anapopata mali, anaruhusiwa kumwoa Amali.

(iv) Ubinafsi

- Mamake Amali – alipenda mali (alipogundua kuwa msimulizi ni tajiri).
- Amali hampingi mamake / haingilii.
- Familia yote ya Amali inapanga harusi bila kumhusisha Amali.
- Orodha ya vitu vya thamani

(v) Bidii / juhudi katika kazi.

- Msimulizi anafanya bidii ili aoe.
- Anaendeleza bidii akiwa Arabuni.
- Anatajirika na kupeleka posa mara ya pili.

(vi) Mila na desturi

- Mila zinakwamiza watu / zinawanyima watu haki k.m. mila ya mahari.
- Mjomba huhusishwa katika maswali ya ndoa.
- Matumizi ya nyimbo katika arusi – maana fiche.
- Bwana arusi anatozwa kiingilio / mahari.

(vii) Nafasi ya mwanamke katika jamii – anachaguliwa mume.

(viii) Nafasi ya wazazi katika ndoa ya wanao – wanamchagulia mume Amali.
(kutaja-1, kueleza 1 = 2) (zozote 6x2=alama 12)

8. (a)

- Huwa na fanani / msimulizi anayeonana ana kwa ana na hadhira yake.
- Huwa na hadhira mahususi / maalum – hadhira tendi / hai.
- Ina wahusika maalumu – binadamu, wanyama au viumbe wengine.
- Huwa na fomula – funguzi / kuanzia – fungia / kumalizia.
- Husambazwa / huwasilishwa kwa njia ya mdomo.
- Huambatana na utendaji / uigizaji – matumizi ya maleba.
- Huwa na wakati wa mazingira maalum ya uwasilishaji wake – asubuhi, usiku.
- Hurithjswa kutoka kikazi kimoja hadi kingine.
- Hapo awali, zilihifadhiwa akilini / kumbukizi / nyoyoni na katika mazingira.
- Hubadililika – hutegemea hadhira, wakati n.k.
- Huzaliwa, hukua na kufa.
- Ina historia ndefu – ni kongwe. (zozote 5x1 = alama 5)

(b)

- Maandishi – kwenye vitabu / majarida.
- Kupitia picha – kamera.
- Sinema / video / filamu.
- Tepurekoda / vinasa sauti / kanda za kunasa sauti.
- Diski za kompyuta / Diski tepetevu. (za kwanza mbili) (2x1 = alama 2)

(c)

- Huzuka na kutoweka / hubuniwa na kutoweka baada ya muda k.m. manyanga.
- Baadhi ya misimu husanifishwa na kukubaliwa katika lugha sanifu k.m. toa chai – hongo.
- Hujikita katika vikundi mbalimbali vya wanajamii k.m. vijana.
- Hutumia lugha ya kimafumbo k.m. machozi ya simba – pombe.
- Huwa na maana tofauti kutegemea wahusika na eneo / Hupata maana kutoka kwa watumiaji / muktadha. Hutumiwa na wanajamii katika mawasiliano yao katika kipindi fulani cha wakati / mahali maalum.
- Misimu si semi sanifu. (zozote 7x1 = alama 7)

(d)

- Kupitia utohozi / kugeuza mpangilio.
- Kwa kufupisha maneno.
- Kutumia ufananisho / sitiari – nyani, kasuku, nyoka.
- Kubadilisha maana ya kawaida ya maneno – toboa.

- Uvumbuzi wa maneno mapya – zii.
- Kuchanganya lugha – kurelax.